

HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA

MUHTASARI WA KIKAO MAALUMU CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFAANYIKA TAREHE 15/10/2021

WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

1.	Justine Bundu	Afisa Mazingira	Mwenyekiti
2.	Gilbeth Martine	Afisa Manunuzi	Katibu
3.	Mohamed Atiki	Afisa Maendeleo ya Jamii	Mjumbe
4.	Rehema Nyoka	Afisa Elimu Msingi	Mjumbe
5.	Andreas Whero	Mwanasheria	Mshauri / Mwanasheria

WAALIKWA:

1.	Ambrose Majumba	Mweka Hazina	Mwalikwa
2.	Dr. Ally Mjema	Mganga Mkuu	Mtumiaji
3.	Qs. Amiry Mchumbuye	Mhandisi wa Wilaya	mwalikwa

AGENDA:

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda za Kikao.
3. Kupokea taarifa ya ujio wa fedha za COVID 19, kuthibitisha nyaraka za Manunuzi na Kupitisha njia ya manunuzi.
4. Kufunga kikao.

AGENDA NA.1. KUFUNGUA KIKAO.

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Kikao kilifunguliwa mnamo saa 10:30 asubuhi. Aidha, aliwashukuru wajumbe kwa mahudhurio mazuri na kufika kwa muda muafaka. Pia aliwakaribisha wajumbe kushiriki katika mijadala kwa kadiri ajenda zitakavyokuwa zinawasilishwa.

AGENDA NA.2. KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO

Agenda za kikao zilithibitishwa.


AGENDA NA.3. KUPOKEA TAARIFA YA UJIO WA FEDHA ZA COVID 19, KUTHIBITISHA NYARAKA ZA MANUNUZI NA KUPITISHA NJIA YA MANUNUZI.

Katibu aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri imepokea fedha kiasi cha Tsh. 1,410,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 42 ya shule za Sekondari, 24 kwa ajili ya Shule shikizi za Msingi na nyumba moja ya 3 kwa 1 ya watumishi wa Idara ya Afya. Aidha, alieleza Tsh. 840,000,000.00 kwa ajili ya sekondari, Tsh. 480,000,000.00 kwa ajili ya Elimu msingi na tsh.

90,000,000.00 kwa ajili ya nyumba ya Idara ya afya. Pia, alieleza kitengo cha usimamizi wa manunuzi kinapendekeza njia ya manunuzi itumike *Force Account*. Baada ya maelezo hayo mwenyekiti alimkaribisha Mwenyekiti. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe ambapo walijadili na kuidhinisha nyaraka za Manunuzi ikiwamo na njia ya Force account kutumika katika ujenzi wa Miradi hii.

AGENDA NA. 3: KUFUNGA KIKAO:

Mwenyekiti alifunga kikao saa 6:45 mchana huku akikisisitiza taratibu zinazofuata zifanyike mapema.


Justine Bundu
Mwenyekiti


Gilbert Martine
Katibu

Umethibitishwa tarehe ...15/10/2021

MATIHURIO YA KIKAO MAAJUM CHA
BODI YA ZABUNI CHA TARIFE 15/10/2021

No.	JINA	CHEO	SAINI
1.	JUSTIN BUNDU	MUMFLETI	Jandu
2.	Giloth Martine	Katibu	Aratine
3.	Mohamed Atiki	Njumba	Atiki
4.	REHEMA NYOKA	MJUMBE	Nyoka
5.	Andreas Wase	Mwamasheria	Wase